*Mulika, Na. 44 (1), 114-137*
*Jarida la Taasisi ya Taaluma za Kiswahili*
*Chuo Kikuu cha Dar es Salaam*

# Uambikaji wa Viambishi Ngeli katika Nomino Sahili Zinazorejelea Ndugu na Maana yake katika Sarufi ya Kiswahili

*Fabiola Hassan*[1]

DOI: https://doi.org/10.56279/mulika.na44t1.7

**Ikisiri**

Nomino sahili ni maneno ambayo kimofolojia yameundwa na mofu huru moja. Pia, kisematiki, maneno haya yana maana zake katika kamusi. Licha ya kuwa na sifa hizi, uambikaji wa viambishi ngeli {*m-*/*mu-*, *ji-*, *ma-*, *ki-*, *ka-*, *tu*, na *u-*} katika nomino hizi unaathiri sifa tajwa. Makala haya yanafafanua athari za kimofolojia na za kisemantiki za uambikaji wa viambishi ngeli katika nomino hizi na maana ya athari hizo katika ufafanuzi wa sarufi ya Kiswahili. Data zilizotumika zilipatikana kwa njia ya ushuhudiaji shiriki, hojaji na usaili. Data hizo zilifafanuliwa kwa kutumia Nadharia ya Matumizi iliyoasisiwa na Lodwig Wittgenstein (1953). Kutokana na data hizo, makala yanaonesha kwamba uambikaji wa viambishi ngeli kwenye nomino hizi husababisha athari za kimofolojia kama vile kuongeza idadi ya mofu kutoka moja kuwa mbili na kubadili aina ya nomino kimuundo. Vilevile, uambikaji huo huathiri maana ya nomino hizo kisarufi na kileksika kwa kuzingatia matumizi yake. Iwapo nomino hizi zitaendelea kupata mashiko na kisha kusanifiwa, athari tajwa zinadokeza mahitaji ya kuboresha uainishaji wa ngeli za nomino, uandikaji wa taarifa za vidahizo katika kamusi na ufafanuzi wa upanuzi na mabadiliko ya maana katika sarufi ya Kiswahili. Hivyo, imehitimishwa kwamba athari za kimofolojia na kisemantiki zinazotokana na uambikaji wa viambishi ngeli katika nomino sahili zinadhihirisha mabadiliko ya lugha na kwamba mabadiliko haya yanapaswa kuzingatiwa katika ufafanuzi wa sarufi ya Kiswahili. Kutokana na matokeo haya, imependekezwa kwamba zifanyike tafiti kuhusu uambikaji wa viambishi ngeli katika nomino sahili za makundi mengine ya nomino katika lugha ya Kiswahili.

## 1.0 Utangulizi

Uambikaji ni mchakato wa kimofolojia wa kupachika viambishi kabla, katikati au baada ya mzizi wa neno ili kuongeza dhana za kisarufi katika neno au kuunda neno jipya (TUKI, 2019). Mchakato huu umefafanuliwa na wanaisimu mbalimbali (taz. Nkwera, 1978; Khamis, 1985; Dresser, 1989; Anderson, 1992; Katamba, 1993; Aronoff, 1994; Rubanza, 1996; Spencer na Zwicky, 1998; Kihore na wenzake, 2001; Peterson, 2008; Kahigi, 2009; Gawasike, 2012; Wesana-Chomi,

[1] Mhadhiri Mwandamizi, Idara ya Kiswahili, Chuo Kikuu cha Dodoma. Baruapepe: fabiola.hassan@udom.ac.tz

2013; Philipo, 2018; TUKI, 2019, Hassan, 2022 na Kombe, 2024). Wataalamu hawa wameeleza kwamba kuna uambikaji wa uambatizi na ule wa unyambuzi. Uambikaji wa uambatizi ni mchakato wa kupachika viambishi kwenye mzizi wa neno ili kuongeza dhana za kisarufi katika neno. Uambikaji huu unahusisha viambishi vya uambatizi. Mifano ya viambishi hivi katika nomino ni vya ngeli na idadi. Kwa upande mwingine, uambikaji wa unyambuzi ni mchakato wa kupachika viambishi kwenye mzizi wa neno ili kuunda neno jipya. Uambikaji huu unahusisha viambishi vya unyambuzi. Mifano ya viambishi hivi katika nomino ni vya unominishi. Hata hivyo, Kombe (2024) anaeleza kwamba hakuna mpaka dhahiri baina ya viambishi vya uambatizi na vile vya unyambuzi. Hii ni kwa sababu kiambishi kimoja kinaweza kufanya kazi ya uambatizi na unyambuzi kwa wakati mmoja. Aidha, pamoja na ufafanuzi huu kuhusu dhana na aina, bado kuna masuala ambayo hayako wazi kuhusu mchakato wa uambikaji. Miongoni mwa masuala hayo ni athari za uambikaji wa viambishi na maana ya athari hizo katika ufafanuzi wa sarufi ya lugha. Hivyo, lengo kuu la makala haya ni kuchanganua athari za uambikaji wa viambishi ngeli katika nomino zinazorejelea ndugu na maana ya athari hizo katika ufafanuzi wa sarufi ya Kiswahili.

Viambishi ngeli ni vile vinavyodokeza kundi la nomino kimofolojia. Viambishi hivi vinapoambikwa kwenye mzizi au shina la nomino, vinaongeza dhima ya kisarufi ya kutambulisha kundi ambalo nomino husika inatokea kimofolojia, yaani ngeli. Jedwali Na. 1 linaonesha viambishi ngeli pamoja na mifano ya nomino.

**Jedwali Na. 1: Ngeli za Nomino katika Lugha ya Kiswahili**

| Ngeli | Viambishi Ngeli | Mifano ya Maneno |
|---|---|---|
| 1. Umoja | mu-/mw-/m- | muuguzi, mwalimu, mtoto |
| 2. Wingi | wa- | wauguzi, walimu, wasichana |
| 3. Umoja | mu-/m- | muongo, mpera, mpapai |
| 4. Wingi | mi- | miongo, mipera, mipapai |
| 5. Umoja | ji-/ø- | jino, jiko, pera, embe |
| 6. Wingi | ma- | meno, meko, mapera, maembe |
| 7. Umoja | ki-/ch- | kiti, kikombe, chumba |
| 8. Wingi | vi-/vy- | viti, vikombe, vyumba |
| 9. Umoja | n-/mb-/ng- | ndizi, nguo, mbuzi |
| 10. Wingi | n-/mb-/ng- | ndizi, nguo, mbuzi |
| 11. Umoja | (l)u- | ubao, uzi, ukuta, udevu, unyasi |
| 12. Umoja | *ka | katoto, kasichana |

| Ngeli | Viambishi Ngeli | Mifano ya Maneno |
|---|---|---|
| 13. Wingi | *tu | tutoto, tusichana |
| 14. | U | usingizi, ugonjwa, upole |
| 15. | ku- | kucheza, kuimba, kulala |
| 16. | Pa- | (*pahala) nyumbani |
| 17. | ku- | (*kwahala) nyumbani |
| 18. | Mu- | (*mwahala) nyumbani |

**Chanzo:** Hassan (2022)

Jedwali Na. 1 linaonesha viambishi vya ngeli katika lugha ya Kiswahili. Mathalani, katika nomino m-toto, kiambishi {m-} kinawakilisha ngeli ya kwanza umoja. Hivyo, nomino za Kiswahili zimewekwa katika ngeli mbalimbali kwa kuzingatia maumbo ya nomino hizo.

Tafiti tangulizi zinaeleza kwamba, kimofolojia, nomino zote zinazoanza na kiambishi fulani kimoja au kinachofanana nazo huwekwa katika ngeli moja kimofolojia (Nkwera, 1978; Khamis, 1985; Rubanza, 1996; Kihore na wenzake, 2001; Peterson, 2008; Gawasike, 2012; Wesana-Chomi, 2013; Philipo, 2018, na Hassan, 2022). Kwa mfano, nomino za ngeli ya kwanza umoja zinaanza na viambishi ngeli {mu-/mw-/m-} na zile za ngeli ya pili wingi zinaanza na {wa-}. Hata hivyo, Hassan (2022) anaeleza kwamba zipo nomino zinazowekwa katika ngeli bila kudhihirisha kiambishi cha ngeli inayohusika. Nomino hizo zinawekwa katika ngeli kwa kuzingatia kigezo cha kisemantiki (maana) au kisintaksia (upatanishi wa kisarufi). Kwa kuzingatia maelezo ya Hassan (2022), mifano ya nomino hizo ni nomino sahili zinazorejelea ndugu kama vile baba, mama, kaka, dada, bibi, babu na shangazi. Nomino hizi zimewekwa katika ngeli ya kwanza umoja na ngeli ya pili wingi ingawa hazianzi na viambishi ngeli vya ngeli husika. Nomino hizi zimewekwa katika ngeli hizo kwa sababu, kisemantiki, zinahusu binadamu au viumbe hai. Pia, kisintaksia zinachukua kiambishi cha upatanishi wa kiima cha ngeli ya kwanza umoja kk1- {a-} na cha ngeli ya pili wingi {wa-}.

Nomino zinazorejelea ndugu ni zile ambazo virejelewa vyake ni ndugu wa damu katika familia. Kwa kuzingatia maelezo ya Hassan (2022), nomino sahili, kimofolojia hazina kiambishi cha ngeli ya kwanza umoja wala cha ngeli ya pili wingi na kisemantiki zina maana zake za kileksika. Kwa mfano, mama ni mzazi wa kike (TUKI, 2019). Hata hivyo, katika matumizi mbalimbali ya lugha, watumiaji lugha wanasawazisha nomino hizi kwa kuambika viambishi ngeli ili zifanane na nomino za ngeli ya kwanza umoja, ngeli ya pili wingi au ngeli nyingine. Mathalani, wanaambika viambishi {mu-/m-} kupata nomino mbaba/mubaba, mmama na mkaka katika umoja na wingi. Pia, wanaambika kiambishi {wa-} ili kupata nomino wababa, wamama na wakaka katika wingi.

Uambikaji wa viambishi ngeli katika nomino zinazorejelea ndugu ni mchakato unaoibua maswali kuhusu athari zake kimofolojia na kisemantiki, pamoja na maana ya athari hizo katika ufafanuzi wa sarufi ya Kiswahili. Kimofolojia, nomino zinazorejelea ndugu zimeundwa na mofu moja na zimewekwa katika ngeli ya kwanza umoja au wingi. Uambikaji wa viambishi ngeli hubadilisha mofolojia ya nomino hizi. Vilevile, kisemantiki nomino hizi zina maana zake za kileksika. Uambikaji wa viambishi ngeli huongeza dhana nyingine za kisarufi au huunda maneno mapya katika Kiswahili. Hivyo, uambikaji wa viambishi ngeli katika nomino zinazotaja ndugu una athari za kimofolojia na kisemantiki ambazo hazikufafanuliwa na wanaisimu tangulizi. Aidha, athari hizo zina maana katika ufafanuzi wa sarufi ya Kiswahili ambayo mpaka sasa imefafanuliwa bila kuzingatia athari za uambikaji wa viambishi ngeli katika nomino zinazotaja ndugu. Kwa hiyo, lengo la makala haya ni kufafanua athari za kimofolojia na za kisemantiki za uambikaji wa viambishi ngeli katika nomino zinazotaja ndugu. Vilevile, makala haya yameeleza maana ya athari hizo katika ufafanuzi wa sarufi ya Kiswahili. Data zilizotumika katika makala haya zilipatikana kupitia mbinu mbalimbali kama ilivyofafanuliwa katika sehemu 2.0.

## 2.0 Methodolojia

Utafiti uliozaa makala haya ulifanyika katika Chuo Kikuu cha Dodoma, Tanzania. Eneo hili lilichaguliwa kama kiwakilishi cha maeneo mengine ambako Kiswahili kinatumika katika mawasiliano rasmi na yasiyo rasmi. Data zilizotumika zilikusanywa kutoka kwa watoataarifa 14 ambao ni wahadhiri (2) na wanafunzi (12) wa taaluma za mofolojia na semantiki na pragmatiki ya Kiswahili kwa ngazi ya umahiri. Data hizo zilikusanywa kwa kutumia mbinu ya ushuhudiaji shiriki, hojaji na usaili. Aidha, mtafiti alitumia usampulishaji lengwa akiwakusudia wahadhiri na wanafunzi wa mofolojia na semantiki na pragmatiki ya Kiswahili kwa sababu wana maarifa kuhusu taaluma hizo. Hivyo, mtafiti alitarajia kupata data toshelevu kutoka kwao. Ili kupata watoataarifa 14, mtafiti alitumia usampulishaji wa kutegemea fursa. Katika mbinu hii, mtafiti alikusanya data kutoka kwa watoataarifa waliokuwa tayari kujaza hojaji au kusailiwa. Idadi ya watoataarifa 14 ilifikiwa baada ya kupata data toshelevu, na kwamba hakukuwa na uwezekano wa kupata data mpya.

Katika mbinu ya ushuhudiaji shiriki, mtafiti alitumia mwongozo wa ushuhudiaji shiriki. Mwongozo huo ulimtaka mtafiti kukusanya nomino zinazorejelea ndugu ambazo hazijaambikwa na zile zilizoambikwa viambishi. Kisha, ulimtaka mtafiti kukusanya taarifa za kimofolojia na kisemantiki za nomino hizo kabla na baada ya kuambikwa viambishi ngeli katika miktadha yake ya matumizi. Mwongozo huo ulimsaidia mtafiti kupata data zinazohusu athari za kimofolojia na za kisemantiki za uambikaji wa viambishi vya ngeli katika nomino zinazotaja ndugu. Mbinu ya hojaji ilihusisha wanafunzi 12. Mtafiti aliandaa hojaji kwa kutumia nomino zilizotokana na ushuhudiaji shiriki. Hojaji hiyo ilikuwa na jozi ya sentensi (a na b)

ambazo ndani yake nomino teule zimetumika. Sentensi (a) zilikuwa zimetumia nomino hizo bila kuambikwa viambishi na sentensi (b) zilikuwa na nomino hizo zikiwa zimeambikwa viambishi ngeli. Watoataarifa walitakiwa kueleza sifa za kimofolojia za nomino iliyopo katika sentensi (b) ambazo hazikuwapo katika nomino iliyopo katika sentensi (a). Pia, walitakiwa kueleza sifa za kisemantiki za nomino iliyopo katika sentensi (b) ambazo hazidhihirishwi na nomino iliyopo katika sentensi (a). Mbinu hii ilimwezesha mtafiti kupata data kuhusu athari za kimofolojia na za kimaana za uambikaji wa viambishi ngeli katika nomino teule. Mbinu ya usaili ilitumiwa baada ya kukusanya data za ushuhudiaji shiriki na hojaji. Katika mbinu hii, mtafiti aliandaa mwongozo wa usaili na kufanya usaili kwa wahadhiri 2. Mwongozo huo ulikuwa na swali lililolenga kujua maana ya athari hizi za kimofolojia na kimaana katika sarufi ya Kiswahili. Mbinu hii ilimwezesha mtafiti kupata data kuhusu maana ya athari hizo katika sarufi ya Kiswahili.

Baada ya kukusanya data, uchambuzi wa data ulifanywa kama ifuatavyo. Ili kupata majibu ya data kuhusu athari za kimofolojia za uambikaji wa viambishi ngeli katika nomino teule, mtafiti alizipanga data hizo katika makundi yenye mfanano wa athari za kimofolojia. Aidha, ili kupata majibu kuhusu athari za kisemantiki za uambikaji wa viambishi ngeli katika nomino teule, mtafiti alizipanga data hizo katika makundi kwa kuzingatia mfanano wa athari za kisemantiki. Baada ya kuziweka katika makundi yenye mfanano wa athari za kimofolojia na kisemantiki, mtafiti alipata data kuhusu athari za kimofolojia na za kisemantiki za uambikaji wa viambishi ngeli katika nomino teule. Aidha, ili kujua maana ya athari hizo katika sarufi ya Kiswahili, mtafiti alizipanga data katika mfanano wa makundi ya maana. Kwa ujumla, baada ya kuweka pamoja data katika makundi yenye mfanano wa hoja, mtafiti alipata data za athari za kimofolojia na za kisemantiki za uambikaji wa viambishi ngeli katika nomino teule na maana ya athari hizo katika sarufi ya Kiswahili. Vilevile, ufafanuzi wa data ulitumia Nadharia ya Matumizi ambayo imefafanuliwa katika sehemu ifuatayo:

## 3.0 Nadharia ya Matumizi

Data zilizotumika katika makala haya zimefafanuliwa kwa kutumia misingi ya Nadharia ya Matumizi (kuanzia sasa NM). Nadharia hii iliasisiwa na Lodwig Wittgenstein, mwaka 1953. Msingi wake ni uhusishaji wa kiyambo cha lugha na matumizi yake katika lugha (taz. Ullman, 1962; Lyons, 1987; Akmajian na wenzake, 2010 & Wikjaya na Yeniterzi, 2011). Hivyo, katika matumizi mbalimbali ya lugha, watumiaji wa lugha huambika viambishi ngeli katika nomino sahili zinazorejelea ndugu. Uambikaji huo husababisha athari za kimofolojia katika nomino hizo. Pia, nomino hizo hupata athari za kimaana kwa kuzingatia matumizi yake. Aidha, athari za kimofolojia na za kisemantiki zina maana yake katika ufafanuzi wa sarufi ya Kiswahili. Kwa ujumla, NM imesaidia kufasiri data kuhusu athari za uambikaji wa viambishi ngeli katika nomino teule pamoja na maana ya

athari hizo katika sarufi ya Kiswahili. Masuala haya yamefafanuliwa katika sehemu inayofuata.

## 4.0 Uambikaji wa Viambishi Ngeli katika Nomino Sahili Zinazotaja Ndugu katika Kiswahili

Tafiti tangulizi zinaonesha kwamba nomino sahili zinazorejelea ndugu zipo katika ngeli ya kwanza umoja na ya pili wingi (Nkwera, 1978; Khamis, 1985; Rubanza, 1996; Kihore na wenzake, 2001; Peterson, 2008; Gawasike, 2012; Wesana-Chomi, 2013; Philipo, 2018; Hassan, 2022). Kwa kuzingatia maelezo ya Hassan (2022) kuhusu nomino sahili, nomino *baba*, *mama*, *kaka*, *dada*, *babu*, *bibi* na *shangazi* ni mifano ya nomino sahili. Nomino sahili kimofolojia zimeundwa na mofu huru moja ambayo haiwezi kugawanyika zaidi na kuleta maana (Wesana-Chomi, 2013; Phillipo, 2018; Hassan, 2022). Aidha, nomino hizi kisemantiki zina maana zake za msingi ambazo zinatokea katika kamusi. TUKI (2019) inaeleza kuwa *baba* ni mzazi wa kiume, *mama* ni mzazi wa kike na *shangazi* ni dada wa baba. Aidha, *dada* ni ndugu wa kike, *kaka* ni ndugu wa kiume, *babu* ni mzazi wa kiume wa baba au mama na *bibi* ni mzazi wa kike wa baba au mama.

Hata hivyo, data zinaonesha kwamba katika matumizi mbalimbali ya lugha, wazungumzaji wa Kiswahili wanaambika viambishi ngeli kabla ya mizizi ya nomino hizi ili kusawazisha na kuzifanya zifanane kimofolojia na nomino nyingine za ngeli husika kama ilivyo katika lugha nyingine za Kibantu. Jedwali Na. 2 linathibitisha hilo.

**Jedwali Na. 2: Viambishi Ngeli Vinavyoambikwa katika Nomino baba, mama, kaka, dada, shangazi, babu na bibi**

| # | Kiambi-shi Ngeli | Nomino baba | Nomino mama | Nomino kaka | Nomino dada | Nomino shangazi | Nomino babu | Nomino bibi |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 1 | {m-} | m-baba | m-mama | m-kaka | m-dada | m-shangazi | m-babu | m-bibi |
| 2 | {wa-} | wa-baba | wa-mama | wa-kaka | wa-dada | - | wa-babu | wa-bibi |
| | {ma-} | - | - | ma-kaka | ma-dada | ma-shangazi | ma-babu | ma-bibi |
| 3 | {mi-} | mi-baba | mi-mama | mi-kaka | mi-dada | mi-shangazi | mi-babu | mi-bibi |
| 5 | {ji-} | ji-baba | ji-mama | - | - | - | - | - |
| 7 | {ki-} | ki-baba | ki-mama | ki-kaka | ki-dada | ki-shangazi | ki-babu | ki-bibi |
| 8 | {vi-} | vi-baba | vi-mama | vi-kaka | vi-dada | vi-shangazi | vi-babu | vi-bibi |
| 12 | {ka-} | ka-baba | ka-mama | ka-kaka | ka-dada | ka-shangazi | ka-babu | ka-bibi |
| 13 | {tu-} | tu-baba | tu-mama | tu-kaka | tu-dada | tu-shangazi | tu-babu | tu-bibi |
| 14 | {u-} | u-baba | u-mama | u-kaka | u-dada | u-shangazi | u-babu | u-bibi |

**Chanzo:** Utafiti (2024)

Jedwali Na. 2 linaonesha kwamba, katika matumizi mbalimbali ya lugha, viambishi ngeli vinaambikwa kwenye mizizi ya nomino *baba*, *mama*, *kaka*, *dada*, *shangazi*, *bibi* na *babu*. Viambishi hivyo ni kng1{*m-*}, kng2 {*wa-*/*ma-*}, kng3 {*mi-*}, kng5 {*ji-*}, kng7 {*ki-*}, kng7 {*vi-*}, kng12 {*ka-*}, kng13 {*tu-*} na kng14 {*u-*}. Data hii inaonesha kuwa nomino teule zinazotaja ndugu zimebadilika kimofolojia.

Hii ni kwa sababu, hapo awali hazikuwa zimeambikwa viambishi ngeli, lakini sasa viambishi hivyo vimeambikwa kabla ya mizizi ya nomino hizi.

Aidha, imebainika kwamba wazungumzaji wa Kiswahili husawazisha na kuzifanya nomino teule zifanane na nomino nyingine za ngeli husika. Mathalani, nomino za ngeli ya kwanza umoja kama vile *mtoto*, *msichana* na *mkurugenzi* huanza na kiambishi ngeli ya kwanza umoja {*m*-}. Aidha, nomino hizo katika wingi huanza na kiambishi cha ngeli ya pili wingi {*wa*-}, yaani *watoto*, *wasichana* na *wakurugenzi*. Hivyo, katika matumizi yasiyo rasmi ya Kiswahili, uambikaji wa kiambishi cha ngeli ya kwanza umoja kng1{*m*-} kabla ya mizizi ya nomino sahili zinazorejelea ndugu, huzalisha nomino *mbaba*, *mmama*, *mkaka*, *mdada*, *mshangazi*, *mbabu* na *mbibi*. Pia, wazungumzaji wa Kiswahili huambika kiambishi cha ngeli ya pili wingi {*wa*-} katika mizizi ya nomino hizo na hivyo kuzalisha nomino *wababa*, *wamama*, *wakaka*, *wadada*, *wababu* na *wabibi*.

Data zinaonesha kwamba uambikaji wa viambishi ngeli katika nomino hizi teule husababisha athari za kimofolojia na za kimaana katika nomino hizi. Athari hizo zinadokeza kwamba ufafanuzi wa masuala ya kimofolojia na kimaana katika sarufi ya Kiswahili unahitaji kufanyiwa maboresho ili kuzingatia matumizi haya ya lugha. Masuala haya yamefafanuliwa katika sehemu 4.1 - 4.3 kama ifuatavyo:

### 4.1 Athari za Kimofolojia

Haya ni mabadiliko ya sifa za kimofolojia za nomino teule. Kulingana na data zilizokusanywa, imebainika kwamba nomino teule hupokea mabadiliko ya kimaumbo baada ya kuambikwa viambishi ngeli katika matumizi mbalimbali ya Kiswahili. Mabadiliko haya yamefafanuliwa kama ifuatavyo:

#### 4.1.1 Mabadiliko ya Aina ya Nomino Kimofolojia

Mabadiliko haya yanahusu uainishaji wa nomino kimofolojia. Hassan (2022) anaeleza kwamba, kimuundo, nomino za Kiswahili zinaweza kuainishwa katika makundi makuu matatu ambayo ni: nomino sahili, nomino changamani na nomino ambatani. Anaeleza kwamba, nomino sahili ni zile zinazoundwa kwa kutumia mofu moja ambayo inajitosheleza kimuundo na kimaana. Aidha, mofu hiyo haiwezi kugawanyika zaidi na kuleta maana kimofolojia. Mfano wa nomino sahili ni *kaka*. Nomino changamani ni zile zinazoundwa kwa mofu mbili au zaidi. Aidha, mofu hizo huweza kuwa huru au tegemezi. Mofu huru huweza kusimama peke yake bila kuhitaji mofu nyingine. Mifano ya mofu huru ni mizizi sahili na mashina kama vile *mama* na *baba*. Mofu tegemezi ni zile ambazo haziwezi kusimama peke yake na kujitosheleza kimaana. Mofu hizi huhitaji mofu nyingine ili kukamilisha maana ya neno. Mifano ya mofu tegemezi ni viambishi mbalimbali. Mfano wa nomino hizo ni *mtoto*. Nomino ambatani ni zile zinazoundwa kwa kuambatanisha maneno mawili au zaidi. Mfano wa nomino hizo ni *askarikanzu*. Kwa kuzingatia

uainishaji wa Hassan (2022), nomino nyingi zinazorejelea ndugu, kimuundo huwekwa katika kundi la nomino sahili. Ni nomino sahili kwa sababu zimeundwa kwa kutumia mofu moja ambayo inajitosheleza kimaana. Aidha, mofu hiyo haiwezi kugawanyika zaidi katika maumbo madogomadogo yenye maana kimofolojia.

Data zinaonesha kwamba, katika matumizi mbalimbali ya Kiswahili, uambikaji wa viambishi ngeli katika nomino teule hubadili nomino hizo kutoka huru kwenda changamani. Ni nomino changamani kwa sababu zimeundwa kwa kutumia mofu tegemezi (kiambishi) na mofu huru (mzizi). Jedwali Na. 3 lifuatalo linaonesha uainishaji wa nomino hizo.

**Jedwali Na. 3: Uainishaji wa Nomino Kabla na Baada ya Uambikaji wa Viambishi Ngeli**

| Na. | Kiambishi Ngeli | Mofu Kabla na Baada ya Uambikaji | Nomino Kabla na Baada ya Uambikaji | Uainishaji wa Nomino Kimuundo Kabla na Baada ya Uambikaji |
|---|---|---|---|---|
| 1. | {m-} | baba | baba | Nomino sahili |
| | | m-baba | mbaba | Nomino changamani |
| 2. | {wa-} | mama | mama | Nomino sahili |
| | | wa-mama | wamama | Nomino changamani |
| 3. | {ji-} | mama | mama | Nomino sahili |
| | | ji-mama | jimama | Nomino changamani |
| 4. | {ki-} | dada | dada | Nomino sahili |
| | | ki-dada | kidada | Nomino changamani |
| 5. | {vi-} | babu | babu | Nomino sahili |
| | | vi-babu | vibabu | Nomino changamani |
| 6. | {ka-} | bibi | bibi | Nomino sahili |
| | | ka-bibi | kabibi | Nomino changamani |
| 7. | {tu-} | dada | dada | Nomino sahili |
| | | tu-dada | tudada | Nomino changamani |
| 8. | {u-} | mama | mama | Nomino sahili |
| | | u-mama | umama | Nomino changamani |
| 9. | {ma-} + {-ji-} | baba | baba | Nomino sahili |
| | | ma-ji-baba | majibaba | Nomino changamani |

**Chanzo:** Utafiti (2024)

Jedwali Na. 3 linaonesha kwamba kabla ya uambikaji wa viambishi ngeli, nomino *baba*, *mama*, *dada* na *babu* zilikuwa sahili kwa sababu ziliundwa na mofu moja. Baada ya uambikaji wa viambishi hivyo, nomino hizo huwa changamani kwa sababu zinaundwa na mofu mbili ambapo moja ni tegemezi na nyingine ni huru. Mathalani, nomino *mbaba* imeundwa na mofu tegemezi {*m-*} na mofu mzizi {-*baba*}. Hivyo, kwa kuzingatia Nadharia ya Matumizi, uambikaji wa viambishi ngeli katika nomino sahili zinazolejea ndugu huzibadili nomino hizo kuwa

changamani. Nomino hizo changamani zinapata maana kulingana na muktadha wake wa kimatumizi. Mathalani, katika mawasiliano ya mwanamke na mwanaume, nomino *mbaba* inarejelea mpenzi wa kiume mtu mzima na mwenye pesa.

### 4.1.2 Mabadiliko ya Idadi ya Mofu

Mabadiliko haya yanahusu idadi ya maumbo ya nomino za kimofolojia baada ya kuambikwa viambishi vya ngeli za nomino. Kabla ya uambikaji wa viambishi ngeli, nomino ziliundwa na mofu moja. Baada ya uambikaji, nomino hizo huwa na mofu mbili kama inavyoonekana katika Jedwali Na. 4.

**Jedwali Na. 4: Idadi ya Mofu Kabla na Baada ya Uambikaji wa Viambishi Ngeli**

| Na. | Kiambishi Ngeli | Nomino Kabla na Baada ya Uambikaji | Mofu Kabla na Baada ya Uambikaji | Idadi ya Mofu Kabla na Baada ya Uambikaji |
|---|---|---|---|---|
| 1. | {m-} | baba | baba<br>kng1.baba | 1 |
| | | m-baba | m-baba<br>kng1-baba | 2 |
| 2. | {wa-} | mama | mama<br>kng1.mama | 1 |
| | | wa-mama | wa-mama<br>kng2-mama | 2 |
| 3. | {ji-} | mama | mama<br>kng1.mama | 1 |
| | | ji-mama | ji-mama<br>kng5-mama | 2 |
| 4. | {ki-} | dada | dada<br>kng1.dada | 1 |
| | | ki-dada | ki-dada<br>kng7-dada | 2 |
| 5. | {vi-} | babu | babu<br>kng8.babu | 1 |
| | | vi-babu | vi-babu<br>kng8-babu | 2 |
| 6. | {ka-} | bibi | bibi<br>kng1.bibi | 1 |
| | | ka-bibi | ka-bibi<br>kng12-bibi | 2 |
| 7. | {tu-} | dada | dada<br>kng1.dada | 1 |
| | | tu-dada | tu-dada<br>kng13-dada | 2 |
| 8. | {u-} | mama | mama<br>kng1.mama | 1 |

| Na. | Kiambishi Ngeli | Nomino Kabla na Baada ya Uambikaji | Mofu Kabla na Baada ya Uambikaji | Idadi ya Mofu Kabla na Baada ya Uambikaji |
|---|---|---|---|---|
| | | u-mama | u-mama<br>kng14-mama | 2 |
| 9. | {ma-} + {-ji-} | Baba | baba<br>kng1.baba | 1 |
| | | ma-ji-baba | ma-ji-baba<br>kng6-kuk-baba | 3 |

**Chanzo:** Utafiti (2024)

Jedwali Na. 4 linaonesha kwamba uambikaji wa viambishi ngeli {*m-*}, {*wa-*}, {*ji-*}, {*ki-*}, {*vi-*}, {*ka-*}, {*tu-*} na {*u-*} husababisha nomino hizo kuwa na mofu mbili. Mathalani, nomino *baba* ilikuwa na mofu moja {*baba*}, lakini baada ya kuambikwa kng1 {*m-*} na kuwa *mbaba* ikawa na mofu mbili ambazo ni kng1 {*m-*} na mzizi {*-baba*}.

#### 4.1.2.1 Mabadiliko ya Ngeli ya Nomino Kimofolojia

Mabadiliko haya yanahusu kundi la nomino za kimofolojia. Kabla ya uambikaji wa viambishi ngeli, nomino teule hutokea katika ngeli ya 1 umoja au ya 2 wingi. Baada ya kuambikwa viambishi ngeli, katika matumizi mbalimbali ya Kiswahili, baadhi ya nomino hizo hunaingia katika ngeli nyingine ambazo si ya 1 wala ya 2 kama ilivyo katika Jedwali Na. 5.

**Jedwali Na. 5: Mabadiliko ya Ngeli**

| Na. | Kiambishi Ngeli | Nomino Kabla na Baada ya Uambikaji | Mofu za Nomino Kabla na Baada ya Uambikaji | Ngeli ya Nomino Kabla na Baada ya Uambikaji |
|---|---|---|---|---|
| 1. | {ji-} | mama | mama<br>kng1.mama | 1 |
| | | ji-mama | ji-mama<br>kng5-mama | 5 |
| 2. | {ki-} | dada | dada<br>kng1.dada | 1 |
| | | ki-dada | ki-dada<br>kng7-dada | 7 |
| 3. | {vi-} | babu | babu<br>kng1.babu | 1 |
| | | vi-babu | vi-babu<br>kng8-babu | 8 |
| 6. | {ka-} | bibi | bibi<br>kng12.bibi | 1 |
| | | ka-bibi | ka-bibi<br>kng12-bibi | 12 |
| 7. | {tu-} | dada | dada<br>kng1.dada | 1 |

| Na. | Kiambishi Ngeli | Nomino Kabla na Baada ya Uambikaji | Mofu za Nomino Kabla na Baada ya Uambikaji | Ngeli ya Nomino Kabla na Baada ya Uambikaji |
|---|---|---|---|---|
| | | tu-dada | tu-dada<br>kng13-dada | 13 |
| 8. | {u-} | mama | mama<br>kng1.mama | 1 |
| | | u-mama | u-mama<br>kng14-mama | 14 |

**Chanzo:** Utafiti (2024)

Jedwali Na. 5 linaonesha kuwa, kabla ya uambikaji wa viambishi ngeli, nomino *mama*, *dada*, *bibi* na *babu* zinatokea katika ngeli ya 1 umoja au ya 2 wingi. Kutokana na uambikaji wa kng5 {*ji*-}, nomino *mama* inatokea katika ngeli ya 5. Pia, kutokana na uambikaji wa kng7 {*ki*-} nomino *dada* inatokea katika ngeli ya 7. Aidha, kutokana na uambikaji wa kng8 {*vi*-} nomino *babu* ipo katika ngeli ya 8. Vilevile, kutokana na uambikaji wa kng12 {*ka*-}, nomino *bibi* ipo katika ngeli ya 12. Pia, kutokana na uambikaji wa kng13 {*tu*-} nomino *dada* ipo katika ngeli ya 13.Vilevile, kutokana na uambikaji wa kng14 {*u*-}, nomino *mama* ipo katika ngeli ya 14. Hivyo, kwa kuzingatia Nadharia ya Matumizi, uambikaji wa viambishi ngeli katika nomino teule hubadili ngeli za nomino hizo. Adha, nomino hizo zinapata maana kwa kuzingatia muktadha wa matumizi. Mathalani, katika mawasiliano ya watu wanaoshushana thamani, nomino *kidada* inarejelea msichana mdodo asiye na thamani.

Kwa ujumla, sehemu 4.1 imefafanua athari za kimofolojia za uambikaji wa viambishi ngeli za nomino katika nomino zinazorejelea ndugu. Athari hizo ni kubadili aina ya nomino kimofolojia, kuongeza idadi ya mofu na kubadili ngeli ya nomino kimofolojia. Sehemu 4.2 inahusu athari za kisemantiki za mchakato huo.

### 4.2 Athari za Kisemantiki

Mabadiliko haya yanahusu maana za nomino teule. Nomino teule zina maana zake za kileksika. Data katika makala haya zinaonesha kwamba, katika miktadha mbalimbali ya matumizi ya lugha, uambikaji wa viambishi ngeli husababisha mabadiliko ya maana za nomino hizo. Mabadiliko hayo ni haya yafuatayo:

#### 4.2.1 Uongezaji wa Dhana ya Ngeli au Idadi katika Nomino

Mabadiliko haya yanahusu uongezaji wa dhana ya ngeli au idadi katika nomino. Data za utafiti zinaonesha kuwa katika miktadha mbalimbali ya matumizi ya Kiswahili, uambikaji wa viambishi ngeli kabla ya mizizi ya nomino teule huongeza dhana ya ngeli au idadi ambayo haikuwapo awali. Jedwali Na. 6 lifuatalo linathibitisha jambo hili:

**Jedwali Na. 6: Uongezaji wa Dhana ya Ngeli au Idadi katika Nomino Teule**

| Na. | Kiambishi Ngeli | Nomino Kabla na Baada ya Uambikaji | Dhana ya Ngeli Kabla na Baada ya Uambikaji | Dhana ya Idadi Kabla na Baada ya Uambikaji |
|---|---|---|---|---|
| 1 | {m-} | baba | Ngeli ya 1 | Haiko wazi |
| | | m-baba | Ngeli ya 1 | Umoja |
| 2. | {wa-} | baba | Ngeli ya 1 | Haiko wazi |
| | | wa-baba | Ngeli ya 2 | Wingi |
| 3. | {ji-} | mama | Ngeli ya 1 | Haiko wazi |
| | | ji-baba | Ngeli ya 5 | Umoja |
| 4. | {ki-} | dada | Ngeli ya 1 | Haiko wazi |
| | | ki-dada | Ngeli ya 7 | Umoja |
| 5. | {vi-} | babu | Ngeli ya 1 | Haiko wazi |
| | | vi-babu | Ngeli ya 8 | Wingi |
| 6. | {ka-} | bibi | Ngeli ya 1 | Haiko wazi |
| | | ka-bibi | Ngeli ya 12 | Umoja |
| 7. | {tu-} | kaka | Ngeli ya 1 | Haiko wazi |
| | | tu-kaka | Ngeli ya 13 | Wingi |
| 8. | {u-} | mama | Ngeli ya 1 | Haiko wazi |
| | | u-mama | Ngeli ya 14 | Haiko wazi |

**Chanzo:** Utafiti (2024)

Jedwali Na. 6 linaonesha kwamba uambikaji wa kng1 {*m*-} katika nomino *baba* huifanya nomino *mbaba* kubeba dhana ya ngeli ya 1 na idadi ya umoja. Pia, uambikaji wa kng2 {*wa*-} katika nomino *baba* huifanya nomino *wababa* kubeba dhana ya ngeli ya 2 na idadi ya wingi. Vilevile, uambikaji wa kng5 {*ji*-} katika nomino *mama* huifanya nomino *jimama* kubeba dhana ya ngeli ya 5 na idadi ya umoja. Aidha, uambikaji wa kng7 {*ki*-} katika nomino *dada* huifanya nomino *kidada* kubeba dhana ya ngeli ya 7 na idadi ya umoja. Pia, uambikaji wa kng8 {*vi*-} katika nomino *babu* huifanya nomino *vibabu* kubeba dhana ya ngeli ya 8 wingi. Aidha, uambikaji wa kng12 {*ka*-} katika nomino *bibi* huifanya nomino *kabibi* kubeba dhana ya ngeli ya 12 na idadi ya umoja. Vilevile, uambikaji wa kng13 {*tu*-} katika nomino *kaka* huifanya nomino *tukaka* kubeba dhana ya ngeli ya 13 wingi. Pia, uambikaji wa kng14 {*u*-} katika nomino *mama* huifanya nomino *umama* kubeba dhana ya ngeli ya 14 bila kuwa na uwazi wa idadi kwamba ni umoja ama wingi. Aidha, uongezaji wa dhana ya ngeli huweza kuunda nomino mpya kileksika kama inavyofafanuliwa katika sehemu 4.2.2.

### 4.2.2 Uundaji wa Nomino zenye Dhana Mpya Kileksika

Haya ni mabadiliko yanayohusu uundaji wa nomino zenye maana mpya za kileksika. Kombe (2024) anaeleza kuwa kiambishi ngeli huweza kuongeza dhana ya kisarufi au kuunda neno jipya lenye dhana mpya ambayo haikuwapo awali. Data katika makala haya zinaonesha kwamba, katika miktadha mbalimbali ya matumizi

ya Kiswahili, uambikaji wa viambishi ngeli kwenye nomino teule huunda nomino zinazorejelea dhana zifuatazo: ukubwa, udogo, udhalilishaji na hali.

Nomino za ukubwaishaji hutokana na uambikaji wa kng5 {*ji-*} katika nomino teule. Hivyo, nomino zinazoundwa hubeba dhana ya ukubwa ambayo haikuwapo katika nomino ya awali kabla ya kuambikwa kwa kiambishi hicho. Jedwali Na. 7 linadhihirisha jambo hili.

**Jedwali Na. 7: Uambikaji wa Kng5 {*ji-*} na Uundaji wa Nomino za Ukubwaishaji**

| **Nomino Kabla ya Uambikaji wa Kiambishi {*ji-*}** | **Maana ya Nomino Kabla ya Uambikaji wa Kiambishi {*ji-*}** | **Nomino Baada ya Uambikaji wa Kiambishi {*ji-*}** | **Maana ya Nomino Baada ya Uambikaji wa Kiambishi {*ji-*}** |
|---|---|---|---|
| mama | mzazi wa kike | ji-mama | mwanamke mwenye umbo kubwa, pengine tofauti na umri wake. |
| baba | mzazi wa kiume | ji-baba | mwanamume mwenye umbo kubwa, pengine tofauti na umri wake. |

**Chanzo:** Utafiti (2024)

Jedwali Na. 7 linaonesha kwamba uambikaji wa kng5 {*ji-*} katika nomino *mama* na *baba* huunda nomino *jimama* na *jibaba*. Kwa kuzingatia NM, nomino *jimama* ina maana ya mwanamke mwenye umbo kubwa, pengine tofauti na umri wake. Kwa upande mwingine, *jibaba* ina maana ya mwanamume mwenye umbo kubwa, pengine tofauti na umri wake. Hivyo, kimatumizi, uambikaji wa kiambishi hiki unazalisha nomino za ukubwaishaji.

Nomino za kushusha thamani hutokana na uambikaji wa kng7 {*ki-*} katika nomino teule. Kwa hiyo, nomino mpya zinazoundwa hubeba dhana ya thamani ndogo ambayo haikuwapo kabla ya kuambikwa kwa kiambishi hicho kama inavyoonekana katika Jedwali Na. 8.

**Jedwali Na. 8: Uambikaji wa Kng7 {*ki-*} na Uundaji wa Nomino za Thamani Ndogo**

| **Nomino Kabla ya Uambikaji wa Kiambishi {*ki-*}** | **Maana ya Nomino Kabla ya Uambikaji wa Kiambishi {*ki-*}** | **Nomino Baada ya Uambikaji wa Kiambishi {*ki-*}** | **Maana ya Nomino Baada ya Uambikaji wa Kiambishi {*ki-*}** |
|---|---|---|---|
| dada | ndugu wa kike | ki-dada | msichana mwenye thamani ndogo, pengine tofauti na umri wake. |
| kaka | ndugu wa kiume | ki-kaka | mvulana mwenye thamani |

| **Nomino Kabla ya Uambikaji wa Kiambishi {*ki*-}** | **Maana ya Nomino Kabla ya Uambikaji wa Kiambishi {*ki*-}** | **Nomino Baada ya Uambikaji wa Kiambishi {*ki*-}** | **Maana ya Nomino Baada ya Uambikaji wa Kiambishi {*ki*-}** |
|---|---|---|---|
| | | | ndogo, pengine tofauti na umri wake. |
| baba | mzazi wa kiume | ki-baba | mwanamume mwenye thamani ndogo, pengine tofauti na umri wake. |
| mama | mzazi wa kike | ki-mama | mwanamke mwenye thamani ndogo, pengine tofauti na umri wake. |
| babu | mzazi wa kiume wa baba au mama | ki-babu | mwanaume mtu mzima mwenye thamani ndogo, pengine tofauti na umri wake |
| bibi | mzazi wa kike wa baba au mama | ki-bibi | mwanamume mtu mzima mwenye thamani ndogo, pengine tofauti na umri wake |

**Chanzo:** Utafiti (2024)

Jedwali Na. 8 linaonesha kwamba uambikaji wa kng7 {*ki*-} katika nomino *dada* na *kaka* huunda nomino za udogoshaji *kidada* na *kikaka*. Kwa kuzingatia NM, katika mawasiliano ya watu wanaoshushana thamani, nomino *kidada* ina maana ya msichana mwenye thamani ndogo. Kwa upande mwingine, nomino *kikaka* ina maana ya kijana mwenye thamani ndogo.

Nomino za udogoishaji hutokana na uambikaji wa kng12 {*ka*-} na kng13 {*tu*-} katika nomino teule. Kng12 huwakilisha umoja na kng13 huwakilisha wingi wa kng12. Kwa hiyo, nomino mpya zinazoundwa hubeba dhana ya udogo ambayo haikuwapo katika nomino za awali kabla ya kuambikwa viambishi hivyo. Jedwali Na. 9 linawasilisha data juu ya jambo hili.

**Jedwali Na. 9: Uambikaji wa Kng12 {*ka*-} na Kng13 {*tu*-} na Uundaji wa Nomino za Udogoishaji**

| **Nomino Kabla ya Uambikaji wa Kiambishi {*ka*-} na {*tu*-}** | **Maana ya Nomino Kabla ya Uambikaji wa Kiambishi {*ka*-} na {*tu*-}** | **Nomino Baada ya Uambikaji wa Kiambishi {*ka*-} na {*tu*-}** | **Maana ya Nomino Baada ya Uambikaji wa Kiambishi {*ka*-} na {*tu*-}** |
|---|---|---|---|
| dada | ndugu wa kike | ka-dada | msichana mdogomdogo, pengine |

| **Nomino Kabla ya Uambikaji wa Kiambishi {*ka*-} na {*tu*-}** | **Maana ya Nomino Kabla ya Uambikaji wa Kiambishi {*ka*-} na {*tu*-}** | **Nomino Baada ya Uambikaji wa Kiambishi {*ka*-} na {*tu*-}** | **Maana ya Nomino Baada ya Uambikaji wa Kiambishi {*ka*-} na {*tu*-}** |
|---|---|---|---|
| | | | kiumbo |
| | | tu-dada | wasichana wadogowadogo, pengine kiumbo |
| kaka | ndugu wa kiume | ka-kaka | mvulana mdogomdogo, pengine kiumbo |
| | | tu-kaka | wavulana wadogowadogo, pengine kiumbo |
| baba | mzazi wa kiume | ka-baba | mwanamume mdogomdogo, pengine kiumbo |
| | | tu-baba | wanaume wadogowadogo, pengine kiumbo |
| mama | mzazi wa kike | ka-mama | mwanamke mdogomdogo, pengine kiumbo |
| | | tu-mama | wanawake wadogowadogo, pengine kiumbo |
| babu | mzazi wa kiume wa baba au mama | ka-babu | mwanamume mtu mzima mdogomdogo, pengine kiumbo |
| | | tu-babu | wanamume watu wazima wadogowadogo, pengine kiumbo |
| bibi | mzazi wa kike wa baba au mama | ka-bibi | mwanamke mtu mzima mdogomdogo, pengine kiumbo |
| | | tu-bibi | wanawake watu wazima wadogowadogo, pengine kiumbo |

**Chanzo:** Utafiti (2024)

Jedwali Na. 9 linaonesha kwamba uambikaji wa kng12 {*ka*-} na kng13 {*tu*-} katika nomino *dada* na *kaka* unazalisha nomino dogoshi *kadada*, *tudada, kababa*, *kamama*, *kabibi*, *kababu*, *kakaka* na *tukaka*. Kwa kuzingatia NM, katika mawasiliano ya watu wanaodoshana, nomino *kadada* ni msichana mdogomdogo na *tudada* ni wasichana wadogowadogo. Aidha, *kakaka* ni mvulana mdogomdogo na *tukaka* ni wavulana wadogo.

Nomino za hali huundwa kutokana na uambikaji wa kng14 {*u*-}. Kng14 huwakilisha dhana ya hali katika nomino. Uambikaji wa kiambishi hiki huunda nomino zenye dhana ya hali ambayo haikuwapo kabla ya kuambikwa kwa kiambishi hicho. Jedwali Na. 10 linawasilisha data zinazobainisha suala hilo.

**Jedwali Na. 10: Uambikaji wa Kng14 {*u*-} na Uundaji wa Nomino za Hali**

| Nomino Kabla ya Uambikaji wa Kiambishi {*u*-} | Maana ya Nomino Kabla ya Uambikaji wa Kiambishi {*u*-} | Nomino Baada ya Uambikaji wa Kiambishi {*u*-} | Maana ya Nomino Baada ya Uambikaji wa Kiambishi {*u*-} |
|---|---|---|---|
| dada | ndugu wa kike | u-dada | hali ya kuwa na tabia za dada |
| kaka | ndugu wa kiume | u-kaka | hali ya kuwa na tabia za kaka |
| baba | mzazi wa kiume | u-baba | hali ya kuwa na tabia za baba |
| mama | mzazi wa kike | u-mama | hali ya kuwa na tabia za mama |
| babu | mzazi wa kiume wa mama au baba | u-babu | hali ya kuwa na tabia za babu |
| bibi | mzazi wa kiume wa mama au baba | u-bibi | hali ya kuwa na tabia za bibi |
| shangazi | dada wa mzazi wa kiume | u-shangazi | hali ya kuwa na tabia za shangazi |

**Chanzo:** Utafiti (2024)

Jedwali Na. 10 linaonesha kwamba uambikaji wa kng14 {*u*-} katika nomino teule huunda nomino *udada*, *ukaka*, ubaba, *umama*, *ubabu* na *ubibi*. Kwa kuzingatia NM, katika mawasiliano yanayohusisha hali au tabia za *dada*, *kaka*, *baba*, *mama*, *babu* au *bibi*, nomino hizi hupata maana za kimuktadha. Mathalani, *udada* ni hali ya kuwa na sifa au tabia za dada kimavazi, matendo au maringo. Kwa upande mwingine, *ukaka* ni hali ya kuwa na tabia za kaka kimavali, matendo na miondoko. Hivyo, nomino zilizoambikwa kng14 {*u*-} hupata maana zake kwa kuzingatia muktadha wake wa matumizi.

### 4.2.3 Mabadiliko ya Maana yenye Mwelekeo Hasi

Haya ni mabadiliko ya maana kutoka kuwa chanya kwenda hasi. Data zilizokusanywa zinaonesha kwamba nomino hizi kabla ya uambikaji wa viambishi ngeli, zina maana zake chanya. Licha ya maana hizo chanya, katika miktadha fulani ya matumizi ya lugha, uambikaji wa viambishi ngeli umezalisha nomino mpya zenye maana hasi kama inavyoonekana katika Jedwali Na. 11.

**Jedwali Na. 11: Mabadiliko ya Maana kutoka Chanya kwenda Hasi**

| Kiambishi Ngeli | Kabla ya ya Uambikaji wa Kiambishi | Maana ya Nomino Kabla ya Uambikaji wa Kiambishi | Nomino Baada ya Uambikaji wa Kiambishi | Maana Hasi ya Nomino Baada ya Uambikaji wa Kiambishi {*u*-} |
|---|---|---|---|---|
| {m-} | baba | mzazi wa kiume | m-baba | mpenzi wa kiume mtu mzima na mwenye pesa, na kwamba baadhi ya wasichana wadogo huwa na mahusiano naye kwa |

| **Kiambishi Ngeli** | **Kabla ya ya Uambikaji wa Kiambishi** | **Maana ya Nomino Kabla ya Uambikaji wa Kiambishi** | **Nomino Baada ya Uambikaji wa Kiambishi** | **Maana Hasi ya Nomino Baada ya Uambikaji wa Kiambishi {*u*-}** |
|---|---|---|---|---|
| | | | | sababu ya pesa zake |
| | shangazi | dada wa baba | m-shangazi | mwanamke mtu mzima na mwenye pesa ambaye hutumia pesa zake kuwarubuni kimapenzi vijana wenye umri mdogo |
| {u-} | mama | mzazi wa kike | u-mama | hali ya mwanaume kuwa na tabia za kike kama vile kulialia bila sababu |

**Chanzo:** Utafiti (2024)

Jedwali Na. 11 linaonesha kwamba nomino *baba* ina maana ya mzazi wa kiume, lakini uambikaji wa kng1 {*m*-} huunda nomino *mbaba*. Nomino *mbaba* ina maana hasi kwamba ni 'mpenzi wa kiume mtu mzima na mwenye pesa na kwamba wasichana wadogo huwa na mahusiano naye kwa sababu ya pesa zake'. Pia, nomino *shangazi* ina maana ya 'dada wa baba', lakini uambikaji wa kng1 {*m*-} huunda nomino *mshangazi*. Nomino *mshangazi* ina maana hasi ambayo ni 'mwanamke mtu mzima na mwenye pesa, ambaye hutumia pesa zake kuwarubuni kimapenzi vijana wenye umri mdogo'. Vilevile, nomino *mama* ni mzazi wa kike, lakini uambikaji wa kng14 {*u*-} huunda nomino *umama*. Nomino *umama* ina maana hasi katika muktadha ambao mwanamume anahusishwa na tabia za kike kama vile kulialia bila sababu'. Hivyo, uambikaji wa viambishi vya ngeli za nomino huunda nomino mpya. Kwa kuzingatia NM, katika muktadha wa uhusishaji wa sifa hasi, uambikaji wa viambishi katika nomino *baba*, *shangazi* na *mama* huzalisha maana hasi. Maana hizo ni tofauti na maana chanya za awali kabla ya kuambikwa viambishi.

### 4.2.4 Upunguaji wa Uzito wa Maana

Haya ni mabadiliko ya maana yanayohusu upunguaji wa thamani ya maana za awali za nomino teule kutokana na uambikaji wa viambishi ngeli. Data zinaonesha kwamba, uambikaji wa viambishi ngeli hupunguza thamani ya maana zake za awali. Hii ni kwa sababu, maana mpya zinazochagizwa na nomino mpya huwa na thamani ndogo zikilinganishwa na maana za awali. Jedwali Na. 12 linaonesha jambo hilo.

**Jedwali Na. 12: Uambikaji wa Viambishi Ngeli na Athari yake katika Upunguaji wa Uzito wa Maana za Nomino Teule**

| Kabla ya Uambikaji wa Kiambishi | Maana ya Nomino Kabla ya Uambikaji wa Kiambishi | Nomino Baada ya Uambikaji wa Kiambishi | Maana ya Nomino Baada ya Uambikaji wa Kiambishi {*u*-} |
|---|---|---|---|
| baba | mzazi wa kiume | m-baba | mpenzi wa kiume mtu mzima na mwenye pesa |
| shangazi | dada wa baba | m-shangazi | mwanamke mtu mzima na mwenye pesa ambaye hutumia pesa zake kuwarubuni kimapenzi vijana wenye umri mdogo |
| kaka | ndugu wa kiume | ki-kaka | mvulana mwenye umbo dogo pengine ni tofauti na umri wake |
| dada | ndugu wa kike | ka-dada | Msichana asiye na thamani |
| mama | mzazi wa kike | u-mama | hali ya mwanamume kuwa na tabia za kike kama vile kulialia bila sababu |

**Chanzo:** Utafiti (2024)

Jedwali Na. 12 linaonesha kwamba nomino *baba* ina maana ya mzazi wa kiume, lakini nomino *mbaba* inapotumiwa na mwanamke ina maana ya mpenzi wa kiume mtu mzima na mwenye pesa. Maana ya nomino *mbaba* ina thamani ndogo ikilinganishwa na maana ya nomino *baba* ambayo ni mzazi wa kiume. Pia, nomino *dada* ina maana ya ndugu wa kike, lakini nomino *kadada* ina maana ya msichana asiye na thamani. Maana ya nomino *kadada* ina thamani ndogo ikilinganishwa na maana ya nomino *dada* ambayo ni ndugu wa kike. Hivyo, kimatumizi, uambikaji wa viambishi ngeli hushusha thamani ya maana za nomino teule.

Hivyo, katika sehemu 4.1 na 4.2, imefafanuliwa kwamba, kabla ya uambikaji wa viambishi, nomino teule zilikuwa na sifa zake za kimofolojia na za kimaana. Kutokana na uambikaji wa viambishi hivyo, sifa hizo hubadilika. Kwa kuwa uambikaji wa viambishi hivi hufanywa na wazungumzaji wa Kiswahili ambao ni wamiliki wa lugha, athari hizi zina maana katika uchanganuzi wa sarufi ya Kiswahili.

### 4.3 Athari za Uambikaji wa Viambishi Ngeli kwenye Nomino Sahili Zinazorejelea Ndugu na Maana yake katika Ufafanuzi wa Sarufi ya Kiswahili

Data zinaonesha kwamba, iwapo maumbo ya nomino hizi pamoja na maana zake vitaendelea kupata mashiko na kisha kusanifishwa, athari za kimofolojia na za kimaana za uambikaji wa viambishi ngeli katika nomino teule za Kiswahili zinadokeza masuala kadhaa katika ufafanuzi wa sarufi ya Kiswahili.

### 4.3.1 Kutokuwa na Mpaka baina ya Uambatizi na Unyambuzi

Hassan (2022) na Kombe (2024) wanaeleza kwamba kuna utata na mwingiliano wa mpaka wa uambatizi na unyambuzi kwa sababu kiambishi kimoja kinaweza kufanya dhima za michakato yote miwili kwa wakati mmoja. Data zinaonesha kwamba, viambishi ngeli vinapoambikwa kwenye nomino teule vinaongeza dhana ya kisarufi ya ngeli au idadi na pia vinaunda maneno mapya kileksika. Hivyo, viambishi vya ngeli vinapoambikwa nomino zinazotaja ndugu vinadhihirisha utata na mwingiliano wa mpaka wa michakato hii miwili kama inavyowasilishwa katika Jedwali Na. 13 lifuatalo:

**Jedwali Na. 13: Mwingiliano wa Uambatizi na Unyambuzi Kutokana na Uambikaji wa Viambishi Ngeli katika Nomino Teule**

| Na. | Kiambishi Ngeli | Nomino Kabla na Baada ya Uambikaji | Dhima ya Uambatizi ya Kiambishi | Dhima ya Unyambuzi ya Kiambishi |
|---|---|---|---|---|
| 1. | {ji-} | mama<br>ji-mama | Kudokeza ngeli ya 5 Umoja | Kuunda neno jipya *jimama* |
| 4. | {ki-} | dada<br>ki-dada | Kudokeza ngeli ya 7, Umoja | Kuunda neno jipya *kadada* |
| 5. | {vi-} | babu<br>vi-babu | Kudokeza ngeli ya 8,<br>Wingi | Kuunda neno jipya *vibabu* |
| 6. | {ka-} | bibi<br>ka-bibi | Kudokeza ngeli ya 12 | Kuunda neno jipya *kabibi* |
| 7. | {tu-} | dada<br>tu-dada | Kudokeza ngeli ya 13 | Kuunda neno jipya *tudada* |
| 8. | {u-} | mama<br>u-mama | Kudokeza ngeli ya 14 | Kuunda neno jipya *umama* |

**Chanzo:** Utafiti (2024)

Jedwali Na. 13 linaonesha kwamba viambishi vya ngeli za nomino vinavyoambikwa kwenye nomino teule huonesha uambatizi na unyambuzi kwa wakati mmoja. Mathalani, uambikaji wa kng14 {*u-*} kwenye nomino *mama* {*umama*} ni uambatizi kwa sababu kiambishi {*u-*} kinadokeza ngeli ya 14. Pia, ni unyambuzi kwa sababu kiambishi hicho huunda neno jipya lenye maana mpya kileksika, yaani *umama*. Matokeo haya ni tofauti na maelezo ya Peterson (2008) na Gawasike (2012) ambao wanatofautisha dhana hizi bila kuonesha utata na mwingiliano wake. Hivyo, wanamofolojia wafafanue uambatizi na unyambuzi huku wakitambua utata na mwingiliano uliopo.

### 4.3.2 Uainishaji wa Ngeli za Nomino Sahili Zinazorejelea Ndugu Kimofolojia

Wanaisimu mbalimbali wameainisha ngeli za nomino za Kiswahili 18 kimofolojia (Rubanza, 1996; Wesana-Chomi, 2013; Hassan, 2022). Katika uainishaji huo, nomino teule zimewekwa katika ngeli ya kwanza umoja na ya pili wingi. Katika ngeli hizo, nomino hizi hazina umbo la ngeli katika umoja wala wingi. Imebainika kwamba watumiaji lugha huambika viambishi ngeli katika nomino teule ili

kuzifanya zifanane kimaumbo na nomino nyingine za ngeli husika. Iwapo nomino teule zilizoambikwa viambishi zitapata mashiko na kusanifishwa, kunapaswa kuwa na maboresho ya uainishaji wa ngeli za nomino kimofolojia kwa kuzingatia maumbo, maana na matumizi ya nomino hizo. Jedwali Na. 14 linawasilisha data za ufafanuzi wa suala hili.

**Jedwali Na. (14): Uainishaji wa Ngeli za Nomino Kutokana na Uambikaji wa Viambishi Ngeli katika Nomino Sahili Zinazorejelea Ndugu**

| Na. | Kiambishi Ngeli/idadi | Mofimu | Mifano ya Nomino | Mifano ya Nomino Mpya |
|---|---|---|---|---|
| 1. | mu-/mw-/m- | Ngeli ya 1 umoja | muuguzi, mwalimu, mtoto | mbaba, mmama, mkaka mdada, mbibi, mbabu |
| 2. | wa- | Ngeli ya 2 wingi | wauguzi, walimu, wasichana, wababa, wamama | wababa, wamama, wakaka, wadada, wabibi na wababu |
| 3. | mu-/m- | Ngeli ya 3 umoja | muongo, mpera, mpapai | - |
| 4. | mi- | Ngeli ya 4 wingi | miongo, mipera, mipapai | - |
| 5. | ji-/ø- | Ngeli ya 5 umoja | jino, jiko, pera, embe, jimama, jibaba | jibaba, jimama, jibabu, jibibi, jikaka na jidada |
| 6. | ma- | Ngeli ya 6 wingi | meno, meko, mapera, maembe | majibaba, majimama majibabu, majibibi, majikaka na majidada |
| 7. | ki-/ch- | Ngeli ya 7 umoja | kiti, kikombe, chupa, chumba | kibaba, kimama, kibabu kibibi, kikaka na kidada |
| 8. | vi-/vy- | Ngeli ya 8 wingi | viti, vikombe, vyupa, vyumba | vibaba, vimama, vibabu, vibibi, vikaka na vidada |
| 9. | n-/mb-/ng'- | Ngeli ya 9 umoja | ndizi, nguo, mbuzi | - |
| 10. | n-/mb-/ng'- | Ngeli ya 10 wingi | ndizi, nguo, mbuzi | - |
| 11. | (l)u- | Ngeli ya 11 | ubao, uzi, ukuta, udevu, unyasi | - |
| 12. | *ka | Ngeli ya 12 | katoto | kababa, kamama, kababu, kabibi, kakaka na kadada |
| 13. | *tu | Ngeli ya 13 | tutoto | tubaba, tumama, tubabu, tubibi, tukaka na tudada |

| Na. | Kiambishi Ngeli/idadi | Mofimu | Mifano ya Nomino | Mifano ya Nomino Mpya |
|---|---|---|---|---|
| 14. | U | Ngeli ya 14 | usingizi, ugonjwa, upole | ubaba, umama, ubabu ubibi, ukaka na udada |
| 15. | ku- | Ngeli ya 15 | kucheza, kuimba, kulala | - |
| 16. | Pa- | Ngeli ya 16 | (*pahala) nyumbani | - |
| 17. | ku- | Ngeli ya 17 | (*kwahala) nyumbani | - |
| 18. | Mu- | Ngeli ya 18 | (*mwahala) nyumbani | - |

**Chanzo:** Utafiti (2024)

Jedwali Na. 14 linaonesha kwamba awali nomino teule ziliwekwa katika ngeli ya 1 na 2. Baada ya uambikaji, zinaingizwa ngeli tofautitofauti. Nomino *mbaba* inaingia katika ngeli ya 1 umoja, *wababa* inaingia katika ngeli ya 2 wingi, *jibaba* inaingia katika ngeli ya 5 umoja, *kibaba* inaingia katika ngeli ya 7 umoja, *vibaba* inaingia katika ngeli ya 8 wingi, *kababa* inaingia katika ngeli ya 12, *tubaba* inaingia katika ngeli ya 13 na *ubaba* inaingia ngeli ya 14. Hivyo, wanamofolojia wahusishe mabadiliko haya katika uchanganuzi wao.

### 4.3.3 Mabadiliko ya Maana

Mtazamo wa wanaisimu tangulizi ni kwamba, mabadiliko ya maana hutokea kileksika na siyo kisarufi (Ullman, 1962; Kibiki, 2012; Kibiki, 2018 na Hassan, 2022). Hii ina maana kwamba, vipashio vidogo ambavyo viko chini ya neno, kama vile viambishi, vinabadili maana ya kileksika na siyo ya kisarufi. Sawa na mtazamo wa wanaisimu hao, imebainika kwamba viambishi ngeli vinapoambikwa kwenye mzizi wa nomino hufanya kazi ya unyambuzi ya kubadili maana ya kileksika ya nomino hizo. Aidha, Hassan (2022) anaeleza kuwa suala hili limedokezwa pia na Bybee (1994) pamoja na Narrog (2012) ambao nao wanadai kwamba vipashio vidogo kuliko neno husababisha mabadiliko ya maana kileksika. Jambo hili linaoneshwa katika Jedwali Na. 15 lifuatalo:

**Jedwali Na. 15: Uambikaji wa Viambishi Ngeli na Mabadiliko ya Maana za Nomino Teule**

| Kiambishi Ngeli | Nomino Kabla na Baada ya Uambikaji | Mifano ya Kabla na Baada ya Uambikaji | Maana Kabla na Baada ya Uambikaji |
|---|---|---|---|
| {m-} | baba | Faraja ana baba yake mzazi. | *baba* ni mzazi wa kiume |
| | m-baba | Faraja ana mbaba mwenye gari. | *mbaba* ni mpenzi wa kiume ambaye ni mtu mzima na mwenye pesa |
| | shangazi | Shangazi amefanana na baba. | *shangazi* ni dada wa baba |
| | m-shangazi | John amepata mshangazi | *mshangazi* ni mwanamke |

| Kiambishi Ngeli | Nomino Kabla na Baada ya Uambikaji | Mifano ya Kabla na Baada ya Uambikaji | Maana Kabla na Baada ya Uambikaji |
|---|---|---|---|
| | | siku hizi. | mwenye tabia ya kuwa na mahusiano ya mapenzi na vijana wadogo wa kiume |
| {u-} | mama | Mama yake Ally ameondoka. | *mama* ni mzazi wa kike |
| | u-mama | Ally ana tabia za umama. | *umama* ni hali ya kuwa na tabia za kike kama vile kulialia |

**Chanzo:** Utafiti (2024)

Jedwali Na. 15 linaonesha kwamba nomino *baba*, *shangazi* na *mama* zikiambikwa viambishi ngeli tunapata maneno mapya yenye maana mpya kileksika. Mathalani, kng1 {*m*-} kikiambikwa kwenye shina la nomino *baba* tunapata nomino *mbaba*. Kwa kuzingatia NM, nomino *mbaba* inapotumiwa na mwanamke inamaanisha mpenzi wa kiume mtu mzima na mwenye pesa nyingi. Maana ya nomino hii ni tofauti na maana ya nomino *baba* ambayo katika kamusi inarejelea mzazi wa kiume. Hivyo, viambishi ngeli vinachagiza mabadiliko ya maana na wanasemantiki wanapaswa kuwa na mtazamo wa Bybee (1994) pamoja na Narrog (2012) kwamba viambishi huchangia mabadiliko ya maana. Athari za uambikaji wa viambishi ngeli hazina maana tu katika mtazamo mpya wa mabadiliko ya maana, pia zina maana katika uandishi wa taarifa za vitomeo vya kamusi kama inavyoelezwa katika sehemu 4.3.4.

### 4.3.4 Uandishi wa Taarifa za Vitomeo vya Kamusi

Katika kamusi zilizopo, taarifa za kimofolojia na maana za nomino teule hazijazingatia mabadiliko ya uambikaji wa viambishi ngeli katika nomino hizi. Mathalani, TUKI (2019) imeonesha kwamba nomino hizi hazina viambishi vinavyotofautisha umoja na wingi kimofolojia. Pia, maana zilizowekwa ni zile zinazozingatia leksimu za maneno haya bila kuambikwa viambishi. Kwa kuwa watumiaji wa lugha wanatambua mabadiliko haya, kuna haja ya kuweka taarifa zinazozingatia athari za kimofolojia na za kimaana za uambikaji wa viambishi ngeli. Mathalani, wanalugha wanajua kwamba kuna utofauti wa idadi baina ya *mbaba* na wababa. Iwapo nomino teule zilizoambikwa viambishi ngeli zitaendelea kupata mashiko na kusanifishwa, maneno haya yaingizwe katika kamusi. Kufanya hivyo kutawasaidia watumiaji wa lugha kupata taarifa za maneno haya katika kamusi. Watumiaji wa lugha wanatarajia wakutane na neno *mbaba* pamoja na kiambishi kinachorejelea wingi {*wa*-}. Aidha, watumiaji wa lugha wanatarajia kukutana na kidahizo *mshangazi* kwa maana ya mwanamke mwenye pesa ambaye anatumia pesa zake kuwa na mahusiano na vijana wadogo kiumri. Kwa kuwa lugha ni mali ya jamii, wanajamii wanapaswa kuzingatiwa pia katika uandishi wa taarifa za kamusi.

**5.0 Hitimisho**

Kwa ujumla, makala haya yamefafanua athari za kimofolojia na za kimaana za uambikaji wa viambishi vya ngeli za nomino zinazorejelea ndugu pamoja na maana ya athari hizo katika ufafanuzi wa sarufi ya Kiswahili. Imeelezwa kwamba nomino hizi zina tabia zake kimofolojia na kimaana. Uambikaji wa viambishi ngeli unaathiri tabia hizo na kuleta mabadiliko ya kimofolojia na kimaana. Athari za kimofolojia ni pamoja na uongezekaji wa mofu kutoka moja kuwa mbili, mabadiliko ya aina za nomino kutoka kuwa sahili na kuwa changamani pamoja na mabadiliko ya namba ya ngeli kutoka ya 1 na 2 kisha kuingia katika ngeli nyingine. Aidha, kimaana imebainika kwamba uambikaji wa viambishi hivyo huongeza dhana mpya za ngeli na idadi katika neno, uundaji wa maneno mapya kileksika, maana zake kubadilika kutoka chanya kuwa hasi pamoja na kupungua kwa uzito wa maana. Pia, imeelezwa kwamba, iwapo nomino hizi teule zitapata mashiko na kusanifiwa, athari hizi za kimofolojia na za kimaana zinadokeza masuala yafuatayo katika sarufi ya lugha ya Kiswahili: kutokuwa na mpaka baina ya uambatizi na unyambuzi, uainishaji mpya wa ngeli za nomino kimofolojia, mtazamo mpya wa mabadiliko ya maana na uandishi wa taarifa za vitomeo iwapo maneno haya yanaendelea kupata mashiko na kusanifiwa kwa ajili ya kuingizwa katika kamusi. Kwa hiyo, kiujumla mabadiliko ya kimofolojia na kimaana ni tabia mojawapo ya lugha ya mwanadamu na kwamba mabadiliko haya yazingatiwe katika ufafanuzi wa sarufi ya Kiswahili.

**Vifupisho na Alama Zilizotumika:**

| | | |
|---|---|---|
| Kng | = | Kiambishi Ngeli |
| NM | = | Nadharia ya Matumizi |
| * | = | Si Kiswahili sanifu |

**Marejeleo**


Akmajian, A., Demers, R.A., Farmer, A.K. na Harnish, R.M. (2010) *Linguistics: An Introduction to Language and Communication* (Toleo la 6). London: The Massachusetts Institute of Technology Press.

Anderson, S. (1992) *A-Morphous Morphology*. Cambridge: Cambridge University Press.

Aronoff, M. (1994) *Morphology by Itself*. Cambridge, Massachusetts: MIT Press.

Gawasike, A. (2012) "Dhana ya Uambikaji katika Kiswahili". *Kioo cha Lugha*, Juz. Na. 10: 70-78.

Hassan, F. (2022) *Mofolojia ya Kiswahili*. Dar es Salaam: Moccony Printing Press.

Kahigi, K.K. (2009) "Unyambulishi wa Nomino na Vitenzi katika Kikahe". *Kioo cha Lugha*, Juz. Na. 7: 1-10.

Katamba, F. (1993) *Morphology*. New York: St. Martin's Press.

Khamisi, A.M. (1985) *Swahili Verb Derivation*. Tasnifu ya Uzamivu (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Hawaii, Hawaii.

Kibiki, J.M. (2012) *Mabadiliko ya Maana katika Vitenzi vya Kiswahili*. Tasnifu ya M.A Kiswahili (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Dar es Salaam.

Kibiki, J.M. (2018) "Mabadiliko ya Maana ya Kitenzi KATA katika Lugha ya Kiswahili". *Kioo cha Lugha*, Juz. Na. 8: 26 – 42.

Kihore, Y.M., Massamba, D.P.B. na Msanjila, Y.P. (2001) *Sarufi Maumbo ya Kiswahili Sanifu* (*SAMAKISA*)*: Sekondari na Vyuo.* Dar es Salaam: TUKI.

Kombe, L.E. (2024) "Utata baina ya Dhana za Unyambulishaji na Uambatizi katika

Ufafanuzi wa Sarufi ya Kiswahili',. *Mwanga wa Lugha*, Juz. Na. 8(2): 69-78.

Lyons, J. (1987) *Semantics*. NewYork: Cambridge University Press.

Matinde, R.S. (2012) *Dafina ya Lugha Isimu na Nadharia: Kwa Sekondari, Vyuo vya Kati na Vyuo Vikuu*. Mwanza: Serengeti Educational Publishers.

Mgullu, R.S. (2002) *Mtalaa wa Isimu: Fonetiki, Fonolojia na Mofolojia ya Kiswahili*. Nairobi: Longhorn.

Mohamed, M.A. (1986) *Sarufi Mpya*. Dar es Salaam: Press and Publicity Center.

Nkwera, F.V. (1978) *Sarufi na Fasihi, Sekondari na Vyuo: Mitaala ya Lugha na Fasihi 4*. Dar es Salaam: Tanzania Publishing House.

Peterson, R. (2008) "Baadhi ya Vipengele vya Uambatizi wa Vitenzi katika Kishambala". *Kioo cha Lugha*, Juz. Na. 7: 52-62.

Philipo, Z.T. (2018) *Utangulizi wa Lugha na Isimu*. Dar es Salaam: Karljamer Publishers Limited.

Rubanza, Y.I. (1996) *Mofolojia ya Kiswahili*. Dar es Salaam: Chuo Kikuu Huria Tanzania.

Spencer, A. na Zwicky, A. (1998) *The Handbook of Morphology*. Oxford: Blackwell Publishers Ltd.

TUKI (2019) *Kamusi ya Kiswahili Sanifu* (Toleo la 4). Nairobi: Oxford University Press.

Ullman, S. (1962) *Semantics: An Introduction to the Science of Meaning*. Oxford: Basil Blackwell.

Wittgenstein, L. (1953) *Philosophical Investigations* (kimefasiriwa na G.E.M. Anscombe). England: Blackwell.